

Tarehe 05.04.2024

**TANGAZO LA ZABUNI YA USOMBAJI WA KAHAWA KUTOKA GHALA LA KEMONDO
HADI TANGA/DAR ES SALAAM MSIMU 2024/2025**

Zabuni na: KCU/Z/2024/2025/08

1. KCU (1990) LTD inakaribisha zabuni ya wasafirishaji wenye magari makubwa (Malori) kwa ajili ya kusomba kahawa kutoka ghala la Kemondo kwenda Tanga/Dar es salaam kwa msimu 2024/2025.
2. Maombi yanakaribishwa kutoka kwa wenye magari yenye uwezo wa kusafirisha tani 30 na magari ni yale yaliyofunikwa sehemu yote ya kubeba mzigo (Box Board Truck).
3. Mwombaji ataje bei kwa tani kwa kilometa zinazozingatia bei elekezi za EWURA.
4. Mwombaji sharti ataje kwa kila gari; aina ya gari, uwezo wake wa kubeba mzigo.
5. Mwombaji awe na leseni ya biashara pamoja na TIN/VAT na SUMATRA.
6. Mwombaji aeleze usalama wa mzigo utakavokuwa wakati akisafirisha kahawa hadi Tanga/Dar es salaam.
7. Wamiliki/waendeshaji ni lazima wawe wameandikishwa kwa mujibu wa sheria ya makampuni.
8. Mwombaji aeleze uzoefu wa kazi alizowahi kufanya.
9. Mwombaji aorodheshe namba za magari yatakayohusika na usombaji/usafirishaji wa kahawa.
20. Maombi yaambatane na ada ya TShs. 100,000/= ambazo hazitarejeshwa kwa mwombaji. Fedha hizo zilipwe kupitia A/C Namba **01J1055955001 KAGERA COOPERATIVE UNION (1990) LTD** iliyopo **CRDB**
10. Tathmini itafanywa kwa kuzingatia vigezo 1-10 vilivyo tajwa hapo juu.
11. Barua za maombi zilizofungwa katika bahasha yenye lakiri na kuandikwa juu yake:-
"MAOMBI YA ZABUNI YA USOMBAJI WA KAHAWA KUTOKA GHALA LA KEMONDO HADI TANGA/DAR ES SALAAM MSIMU 2024/2025" kwa anuani tajwa hapa chini,
MENEJA MKUU,
KCU (1990) LTD,
P.O BOX 5,
BUKOBA.
12. Bahasha hiyo iletwe kwa mkono katika ofisi ya manunuzi KCU (1990) Ltd kabla au mnamo tarehe 19.04.2024. saa 4.00 asubuhi siku ya Ijumaa na ufunguzi wa maombi yote utafanyika muda huo, waombaji au wawakilishi wa waombaji wanaalikwa katika ufunguzi mara tu baada ya saa ya mwisho yakupokea zabuni
13. Maombi yatakayo chelewa, maombi yasiyokamilika, maombi yaliyowasilishwa kwa njia ya kieletroniki na maombi yasiyokuwepo siku ya ufunguzi hayatahusishwa na uchambuzi wa kumpata mzabuni.
Imetolewa na;

MENEJA MKUU
KCU (1990) LTD

